**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA KATIKA SHULE YA SEKONDARI DR SAMIA DODOMA.

**JANUARI, 2026**

**DODOMA**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS-TAMISEMI**

Namba za Simu:

Mkuu wa Shule :
0762594980
0684209902

Dr.Samia-Dodoma Sekondari
S.L.P. 2296

**DODOMA**

23/11/2025

MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI.......................................................

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA KATIKA SHULE YA SEKONDARI DR.SAMIA-DODOMA JANUARI 2026.**

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Kwanza katika shule hii mwaka 2026.

**1.0 MAHALI SHULE ILIPO**

Shule ya Sekondari Dr. Samia_Dodoma ipo umbali wa kilometa 14 Mashariki mwa Mji wa Dodoma. Unapanda bajaji za kwenda Iyumbu zinayopatikana kituo cha mabasi Kimbinyiko ya zamani kwa nauli ya Tsh 1500 hadi Iyumbu kituo cha kwa Anold, panda pikipiki hadi shuleni maarufu kama Iyumbu Mfano. Au ukishuka na mabasi nanenane panda daladala zinazoenda Ihumwa kwa nauli ya Shilingi 500, utashuka kituo cha St Peter Clever na kupanda pikipiki kwa Shiling 2,000 hadi shuleni Dr.Samia. **KARIBU SANA!**

Muhula wa masomo unaanza terehe **13/01/2026** hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **12/01/2026** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **31/01/2026**.

**2.0 Mwanafunzi anatakiwa kuja na mahitaji yafuatayo**

**2.1 Sare za shule**

**Kwa wasichana**

i). Sketi ya vyumbavyumba vyenye mchanganyiko wa rangi nyekundu, nyeupe(off), nyeusi na shati mikono mifupi. Kizibao kinachofanania na kitambaa cha sketi, shati jeupe la mikono mifupi na tai ndefu ya kitambaa cha sketi.

**N.B**

- Sketi ishonwe kwa marinda ya kawaida kati ya 12-15 na iwe ndefu ifike kwenye kifundo cha mguu.

  Epuka kukata kitambaa cha tofauti.

- Waliokaribu wanaweza kupata sampuli ya kitambaa Shuleni Dr. Samia.

iii. Mashati mawili meupe ya mikono mifupi

iv. Sweta la shule 1 rangi nyeusi yenye shingo ya V mbele, lisilo na mchirizi wowote.

v. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi,visiwe na shingo ndefu kama buti.

vi. Soksi jozi za kutosha nyeupe ndefu zisiwe na weusi kwenye unyayo.

vii. T-shirt 1 ya rangi ya kijivu yenye kola iliyo na nembo ya shule (itapatikana shuleni).

viii. Hijab (kijuba) rangi nyeupe ifunike kifua cha mwanafunzi (isifunike tumbo) na kisiwe naurembo.

ix. Sare ya michezo ni sketi solo iliyounganishwa na bukta ya rangi dark blue na tshirt iwe ya mikono mifupi na isiyo ya kola ya rangi nyeusi na ufito mweupe pembeni.

x. Nguo za kushindia (shamba dress) gauni 2 za Solo, ndefu hadi kwenye kifundo cha mguuni rangi ya maroon (damu ya mzee).

xi. Badge (beji) 1 ya bendera ya Taifa.

xii. Track Suit blue bahari yenye mistari mweupe pembeni isiyo na kofia.

xiii. Raba nyeupe kwa ajili ya michezo.

ix. Hijabu za Shamba dress ziwe za rangi ya maroon.

**Wavulana**

i) Suruali mbili rangi ya dark blue iliyokolea ,ishonwe kwa usahihi kwa kuzingatia vipimo sahihi na marinda mawili. Kinyume na hapo atashona nyingine.

ii) Mashati meupe mawili ya mikono mifupi na tai ndefu ya rangi ya suruali

iii) Sweta la shule 1 rangi nyeusi yenye shingo ya V mbele ,lisilo na mchirizi yoyote

iv) Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi ,visiwe na shingo ndefu kama buti.

v) Soksi jozi za kutosha nyeupe zisiwe na weusi kwenye unyayo.

vi) Tshirt ya rangi ya kijivu yenye kola iliyo na nembo ya shule (itapatikana shuleni) kwa sare ya darasani.

vii) Nguo ya kushindia aje na suruali mbili za kijivu na tshirt maroon plain yenye kola.

viii) Badge (beji) 1 ya bendera ya Taifa

ix) Track suit nyeusi yenye mistari mweupe pembeni isiyo na kofia

x) Raba nyeupe kwa ajili ya michezo.

## 2.2. Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni: -

i) Ream 2 za karatasi kwa mwaka.

ii) Saa ya mkononi (**isiwe smart watch**)

iii) Daftari kubwa “counter book” Q3 zisipungue 6, kalamu, penseli,rula,n.k

iv) Godoro la ukubwa wa futi 2 ½ x 6.

v) Vitabu vya kiada vya masomo ya kidato cha kwanza vilivyoandaliwa na Taasisi ya Elimu TIE na vya ziada kadiri mzazi atakavyomudu kupata.

vi) Mashuka pair 2 ya pink kwa wasichana na wavulana shuka pair mbili za blue, blanketi 1, foronya 2 zinazofanana na shuka husika, chandarua nyeupe 1 na mto.

vii) Vyombo vya chakula ni Sare kwa wanafunzi wote hivyo vinapatikana shuleni (sahani, bakuli, kijiko na kikombe)

viii) Viatu vya wazi vya kimasai (culture) kwa ajili ya kushindia. Mwanafunzi haruhusiwi kuvaa ndala au yeboyebo. Ndala zinatumika bafuni na maliwatoni tu.

**Vifaa vya usafi;**

a. Fagio gumu (hard broom) 1,
b. Fagio la chelewa 1 (lenye mpini),
c. Ndoo 2 ndogo zenye mifuniko.
d. Sabuni ya Aro moja
e. Sabuni ya maji Lita 5
f. squizzer moja

xi. Sanduku la chuma (trunker), tochi na betri zake/tochi ya sola.

**ANGALIZO.**

i. Mwanafunzi asije na mizigo au begi kubwa shuleni,aje na tranka moja imara.
ii. Hairuhusiwi mwanafunzi kutembelewa na wageni wakati atakapokuwa shuleni **ISIPOKUWA** kwa wito maalumu wa Mkuu wa Shule. Siku ya kuwaona wanafunzi itatangazwa rasmi.
iii. Ni marufuku mwanafunzi kuja na nguo za nyumbani, Mwanafunzi asafiri na sare ya darasani ya shule hii.Nguo za nyumbani, haziruhusiwi; akija nazo zitateketezwa mara moja.

### 3.0 Sheria na Kanuni za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya Mwaka 1995. Aidha inazingatia

miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Technolojia yenye dhamana ya Elimu na Ofisi ya Rais TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa Elimu nchini.Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;-

**3.1 Sheria na kanuni muhimu za shule**

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote , wanafunzi wengine na jamii kwaujumla ni jambo la lazima.
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku(Preparation)
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa.
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
vi. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
vii. Kuzingatia ratiba ya shule
viii. Kutunza usafi wa mwili,mavazi na mazingira ya shule.
ix. Kutunza mali za shule
x. Ni marufuku kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya Daktari,
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kuja na simu shuleni kwa namna yeyote ile,na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi.
xii. Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala

kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye bweni ambalo hakupangiwa.

xiii. Wanafunzi wote wanatakiwa kunyoa nywele.

**3.2 Makosa yatakayosababisha mwanafunzi kufukuzwa shule ni pamoja na;-**

i. Wizi

ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya **siku 90 bila taarifa/ UTORO**

iii. Kugoma au kuhamasisha mgomo

iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/ walezi na jamii kwa jumla.

v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au na mtu yeyote yule.

vi. Kusuka nywele.Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawaposhuleni.

vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya

viii. Uvutaji wa sigara.

ix. Uasherati, uhusiano wa jinsia moja, kuoa au kuolewa.

x. Kupata ujauzito au kutoa mimba

xi. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za shule na sheria za nchi.

xii. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.

xiii. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.

xiv. Kudharau bendera ya Taifa.

xv. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.

xvi. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

## 4. Viambatisho na Fomu Muhimu

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na

Mganga Mkuu wa hospitali ya serikali.

ii. Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/ mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai. (mkataba huu utapatikana shuleni)

iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni, kulipa ada, michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule. (imeambatishwa ukurasa wa 5)

iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu.

**5. Tafadhali soma kwa makini maelekezo /maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

**MUHIMU**

i. Baada ya kupakua (download) fomu hii, tafadhali jaza jina kamili la mwanafunzi, na anwani y a hapa DR.SAMIA-DODOMA SECONDARY SCHOOL.

ii. Taarifa hizi zijazwe kwenye ukurasa wa kwanza.

iii. Mwanafunzi atakapo ripoti shuleni aje na fomu hii

iv. Mwanafunzi aje na nakala ya cheti cha kuzaliwa

v. Mwanafunzi aje na kadi ya bima ya afya kama anayo.

**KARIBU SANA DR.SAMIA-DODOMA SHULE YA SEKONDARI.**

**Saini ya Mkuu wa Shule:**

***Jina la Mkuu wa Shule:*** **LETICIA J. SINGO**

***Muhuri wa Mkuu wa shule:***

HEADMISTRESS

NOV 2025

DR SAMIA DODOMA SECONDARY SCHOOL
P.O Box 2296
DODOMA

**OFISI YA RAIS-TAMISEMI**

**HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA**

**SHULE YA SEKONDARI DR.SAMIA-DODOMA**

**FOMU YA KUKUBALI SHULE**

## A. SEHEMU YA MWANAFUNZI

1. Mimi (Majina kamili) ………………………………………………………………… Nimekubali kuingia kidato cha……………..DR Samia - Dodoma kuanzia tarehe …………….. hadi nitakapomaliza kidato cha …………..
2. Naahidi kwamba nitatii sheria za Shule na kushiriki katika shughuli zote za shule kikamilifukulingana na ratiba.
3. Tarehe ya kuzaliwa ……………………………….. Kijiji …………………………………… Tarafa ……………………………………………… Wilaya ……………………………… Shule unakotoka …………………………………………Namba yako ya mtihani ……………..
4. Kituo cha gari (Bus) au Gari Moshi kilichopo karibu na nyumbani kwako………………………
5. Nikimaliza kusoma shule ningependa kufanya kazi ifuatayo ……………………………………
   Sahihi ya mwanafunzi ………………………….. Tarehe …………………………………

## B. SEHEMU YA MZAZI AU MLEZI

1. Mimi (majina kamili)………………………………………………………………………ninakubali

   mtoto wangu asome “Dr.Samia kuanzia kidato cha…………………..hadi

   atakapomaliza kidato cha……Nakiri kukubaliana na sheria,kanuni,kulipa ada,michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.
2. Jina kamili la Baba ………………………… Jina kamili la Mama…………………………………

3. Kazi ya Baba .................................. Kazi ya Mama........................

4. Anwani ya Mzazi/Mlezi ...................................

..............................................................................

5. Wafuatao ni Ndugu zake ninaowatambua wanaishi hapa Dodoma na wanaweza kumsaidiawakati wa dharura (picha zao)

| NA. | JINA LA MLEZI/NDUGU | MAHUSIANO | ANAKOISHI | SIMU YAKE |
|---|---|---|---|---|
| 1 | | | | |
| 2 | | | | |
| 3 | | | | |
| 4 | | | | |

6. Madhehebu ya Dini ya Mtoto ni mkristo/muislam(kata lisilohusika) 7. Ripoti zote za maendeleo ya mwanafunzi ziwe zinatumwa kwa

..........................................................................................

Saini ya Mzazi/ Mlezi ........................................... Tarehe ......................................

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**DODOMA CITY COUNCIL**

**DR. SAMIA – DODOMA SECONDARY SCHOOL**

**A FORM FOR STUDENT MEDICAL EXAMINATION**

***To be completed by a Medical Officer***

................................................... (Insert name of the Government Medical

Institution) Name of Student .................................................. Form .....................

Year...............

Age..............................................................Sex...............................

Blood count.........................................................................................

Stool ....................................................................................................

Urine ....................................................................................................

T. B. Test..............................................................................................

Eyes......................................................................................................

Ears......................................................................................................

Chest....................................................................................................

Spleen ..................................................................................................

Abdomen..............................................................................................

Teeth ............................................................................................................

Additional information: - ***(e.g. pregnancy, physical defects, infections, psychological disorder, chronic or family diseases).***

.......................................................................................................................

...........

.......................................................................................................................

...........................................................................................................

**I certify that above pupil is fit to continue with studies in Secondary School for four years.**

Name of Medical Officer ................................................. Signature ................ Designation .....................................

Station & Official Stamp........................................ Date ..................